# IWE NURU

## JANUARI, FEBRUARI, MACHI
## 1982

**JANUARI:** **WANAWAKE WALIOMHUDUMU MUNGU:**

Mwandishi, Mary Small

1. Miriamu
2. Debora
3. Mjane wa Sarepta
4. Mwanamke wa Shunemu

**FEBRUARI:** **WANAWAKE WALIOMHUDUMU MUNGU:**

Mwandishi, Mary Small

1. Elisabeti
2. Ana
3. Salome
4. Wanawake Wawili Waitwao Mariamu

**MACHI:** **WANAWAKE WALIOMHUDUMU MUNGU:**

Mwandishi, Mary Small

1. Juma la Maombi

   Mwandishi, Syd Pearce
2. Prisila
3. Fanny Crosby
4. Lottie Moon

**MISAADA MAALUM:** Mwandishi, Margie Duncan

©
Copyright, 1982
Baptist Publications House
All rights reserved

Published and printed by
Baptist Publications House
Box 30370, Likoni Road, Nairobi



6. Itoe keki yako na uiweke kwenye karatasi safi ili ipoe. Sasa tumia wakati wa chai.

**Mkate wa Unga wa Mahindi**

Vijiko vikubwa 6 vya unga wa mahindi.

Vijiko vikubwa 4 vya unga wa ngano.

Vijiko vikubwa 2 vya sukari.

Vijiko vikubwa 2 vya mafuta ya Kimbo au Blue Band.

Kijiko kidogo 1 cha chumvi.

Vijiko vidogo 3 vya hamila (baking powder).

Mayai 2

Kikombe cha chai 1 cha maziwa.

**Jinsi ya Kutayarisha:**

1. Weka unga na baking powder pamoja kwenye bakuli. Changanya vizuri na chumvi na sukari.
2. Koroga yai vizuri pamoja na maziwa na mafuta.
3. Mwaga huo mchanganyiko kwenye vile vitu vikavu na kukoroga vyote pamoja ukitumia kijiko cha mti.
4. Sasa mwaga kwenye sufuria ndogo au mkebe ambayo umepakwa na mafuta. Jaza kidogo zaidi ya nusu.
5. Weka kwenye jiko lako lililoshika moto kwa dakika 25 au zaidi.
6. Baada ya kuwa tayari weka kwa chombo kingine ili keki yako ipoe. Tumia kwa chai ikiwa moto au imepoa.

Weka mchanganyiko wa keki kwenye mikebe na uweke hiyo mikebe kwenye sufuria cha mchanga. Funika na mfuniko halafu weka makaa juu ya mfuniko. Usifungue fungue mpaka umalize dakika 40 au 60, ndipo utafunua na kutazama keki yako kama ni tayari.

### Mkate wa Njugu

Vijiko vikubwa 2 vya njugu zilizotolewa maganda na kupondwa-pondwa.

Vikombe 1½ vya unga wa ngano.

Vijiko vidogo 2 vya hamila (baking powder).

Robo kijiko kidogo cha chumvi.

Kikombe robo tatu ya maziwa.

Vijiko vikubwa 1½ vya sukari.

**Jinsi ya Kutengeneza:**

1. Changanya unga, baking powder, chumvi na sukari katika bakuli.
2. Koroga yai vizuri kisha changanya na maziwa na kukoroga pamoja. Mwaga hayo maziwa na mayai katika mchanganyiko wa namba ya kwanza.
3. Chukua njugu na kupondaponda. Ongeza katika mchanganyiko huo na koroga vyote pamoja.
4. Chukua mikebe yako na kupaka Blue Band au Kimbo. Baada ya hayo weka huo mchanganyiko ndani ya hiyo mikebe. Weka mahali kwa dakika ishirini (20).
5. Sasa weka katika jiko lako ambalo limeshika moto kwa saa moja.




## UTANGULIZI

Kiini cha masomo yetu ya miezi hii mitatu kitakuwa juu ya "Wanawake waliomhudumu Mungu." Tutajifunza juu ya wanawake walioishi hapo kale. Wengine walikuwa wakiishi miaka ya hivi karibuni. Tutajifunza mambo ya maana kutoka katika maisha yao. Tutajifunza njia ambazo kwazo tungeweza kumtumikia Mungu siku hizi.

Maombi yetu ni kwamba masomo haya yatamsaidia kila mmoja wenu kuwa mwanamke wa Kikristo aliye mzuri zaidi. Mwombeni Mungu ili awaongoze mnapojifunza kurasa hizi kila juma.

3. Tafuta makaa, mikebe ya Kimbo au Blue band au mikebe yo yote yenye mafuta ya kupikia mboga. Mikebe hiyo isiwe mirefu kuzidi sufuria.

4. Tafuta mchanga, au ufukwe.




Hii ni oven ya jiko la makaa na sufuria.

**Jinsi ya Kutengeneza:**

Chukua makaa na kuwasha kwenye jiko. Wakati makaa yanapata moto, changanya vifaa hivi:-

Weka mchanga au ufukwe kwenye sufuria. Weka sufuria kwenye moto na kuifunika ili ipate moto.

I Mkate wa Njugu

II Mkate wa Unga wa Mahindi

Lottie alianza kujimudu. Alishika vidole pamoja kama kuwasalimu wale watu aliowapenda. Ilikuwa katika njia hii, akiwa na tabasamu ya salamu na kulinong'ona jina la rafiki yake, halafu Lottie Moon alikufa.

Yeye alimtumikia Mungu kwa muda mrefu. Alikuwa mwaminifu katika kazi yake.

**Kiongozi:**

Leo tumejifunza juu ya maisha ya Mmisheni Mbatisti aliye mashuhuri. Tunaweza kujifunza mambo fulani kutokana na maisha yake.

Mungu aliposema naye, alitii. Mungu alimjulisha ya kuwa alihitaji kutubu, kisha aokolewe. Naye alimkubali Yesu kuwa Mwokozi wake. Alipojua ya kuwa Mungu alimtaka aende katika nchi ya China, yeye alijibu, "Mimi ni tayari kwenda."

Mungu anaposema nasi siku hizi, ni lazima tumtii. Ni lazima tumtii katika wokovu. Ni lazima tumtii kanisani kwetu na kwetu nyumbani. Pengine hatatuita kwenda kushuhudia katika nchi nyingine. Yeye huwaita Wakristo wote kuwa mashahidi kila mahali walipo.

Na tuombe, "Ee Bwana, mimi ni tayari, kukutii wewe. Nipe nguvu na hekima ili niweze kuufuata uongozi wako."

## MISAADA MAALUM

**Matayarisho:**

1. Tafuta sufuria moja na mfuniko wake.
2. Tafuta jiko la makaa kulingana na sufuria hiyo.





Mpango wa Kwanza

## MIRIAMU

**Kuyasoma Maandiko:** Kutoka 2:1-4

**Kifungu cha Kukumbuka:**

*"Lakini Mungu na ashukuriwe atupaye kushinda kwa Bwana wetu Yesu Kristo."*

*1 Wakorintho 15:57*

**Kiongozi:**

Miriamu ndiye mwanamke wa kwanza katika Biblia ambaye alikuwa akijishughulisha na mambo ya taifa. Yeye alikuwa kiongozi kati ya wanawake wa taifa la Israeli. Leo tutajifunza habari za maisha yake. Pia, leo tutajifunza mambo kuhusu maisha yetu.

**Sehemu ya Kwanza:** Nchi Yake

Watu wa taifa la Israeli walikuwa wakiishi katika nchi ya Misri. Walikuwa watumwa wa watu wa Misri kwa muda mrefu. Walikuwa wakifanya kazi ngumu. Waliendelea kumwamini na kumwabudu Mungu. Naye mtawala wa Misri alianza kuwaogopa watu wa Israeli. Alifikiria walikuwa na nguvu sana wakiwa kama taifa. Kwa hivyo alitoa amri kwa wazalishaji, "...Ikiwa ni mtoto mwanamume, basi mwueni, bali ikiwa ni mtoto mwanamke, na aishi" (Kutoka 1:16b). Wakati amri hii ilipotolewa pengine Miriamu alikuwa msichana mdogo mwenye umri wa miaka saba. Naye alikuwa na ndugu yake aitwaye, Haruni, ambaye pengine alikuwa na umri wa miaka mitatu. Halafu mamaye Miriamu alikuwa na mimba ya mtoto mwingine. Mamaye alimwamini Mungu kuwa atamtunza yeye pamoja na mtoto ambaye alikuwa hajazaliwa.

**Sehemu ya Pili:** Dadake Musa

Wakati uliendelea kupita na mwishowe mwana alizaliwa. Mamaye alimficha huyo mtoto nyumbani kwa muda wa miezi mitatu. Kwa sababu Miriamu alikuwa ndiye mtoto mkubwa, tutaweza kufikiria ya kuwa alimsaidia sana mamaye katika kumtunza Haruni na mtoto mchanga aliyezaliwa.

Wakati uliwadia ambapo yule mama hangeweza kumficha tena yule mtoto, basi alitengeneza kisafina cha kikapu. Akakitengeneza hivi kwamba maji hayangeweza kuingia ndani. Kisha alimweka yule mtoto ndani ya hicho kisafina na kukiweka ndani ya mto. Yule mama alikiweka kile kisafina kati ya manyasi marefu kando ya mto. Naye Miriamu alisimama mbali kidogo ili alinde kile kisafina kilichokuwa na mtoto ndani yake. Miriamu alikuwa mwenye ujasiri. Pia hakuogopa. Yeye pamoja na mamaye walifahamu ya kuwa hapa ni mahali ambapo binti Farao alipokuwa akishuka ili aoge.

Na wakati huo huo binti Farao alishuka ili aoge. Naye alikiona kile kisafina. Mmoja wa wajakazi wake alitumwa kwenda kukileta kile kisafina kutoka majini. Wakati binti Farao alipokifungua kile kisafina alimkuta ndugu mdogo wa Miriamu - yaani Musa.

Miriamu alikimbia kwa haraka kwenda kwake Binti Farao. Naye aliuliza, "Je! niende nikamwite mlezi katika wanawake wa Kiebrania, aje kwako, akunyonyeshee mtoto huyu?" (Kutoka 2:7). Naye binti Farao alijibu, "Haya! enenda." Naye Miriamu alikimbia nyumbani akaenda akamwita mama yake yule mtoto. Mungu aliyajibu maombi ya imani yao. Aliyaokoa maisha ya mtoto Musa.

**Sehemu ya Tatu:** Kiongozi wa Wanawake

Miaka mingi ilipita katika maisha ya wana wa Israeli kabla ya Miriamu kutajwa tena. Biblia haitwambii cho chote kile





**Sehemu ya Tatu:** Katika China

Mara Lottie alianza kujifunza lugha ya watu wa nchi ile. Alikuwa akienda pamoja na wale wamisheni wengine walipotembelea vijiji. Alipokuwa akiwaambia watu habari za pendo la Mungu, alikuwa akiliona jambo moja ambalo kila mmoja wetu huliona siku hizi. Wengine walisikiza vizuri na wakaamini. Na wengine walimkataa Mungu. Lakini hata hivyo aliendelea katika kumtumikia Mungu. Dadaye aliyekuwa mdogo alikuwa ameshawasili China kabla ya Lottie. Kwa muda wa miaka mitatu, baada ya Lottie kufika China dadaye alipata kuwa mgonjwa sana. Lottie alimsindikiza dadaye mpaka nyumbani kwao nchini Amerika. Hatimaye Lottie alirudi kwenye kazi ya Mungu katika China.

Tangu wakati huo mpaka leo, Wabatisti wa Amerika hutoa matoleo katika mwezi wa Desemba. Pesa hizo zote hutumiwa katika kazi ya Umisheni wa Kibatisti katika ulimwengu. Huitwa Matoleo ya Krismasi ya Lottie Moon. Majengo mengi ya makanisa katika nchi hii yetu yamewezekana kujengwa kutokana na matoleo haya.

**Sehemu ya Nne:** Kifo Chake

Lottie alimtumikia Mungu kwa muda wa miaka 39 katika nchi ya China. Akiwa na umri wa miaka 72, alianza safari yake ya mwisho ya kwenda hadi Amerika. Naye alikuwa mgonjwa sana. Alikuwa ameshafanya kazi sana, akiwasaidia watu wa China kumjua Mungu na pendo lake. Watu wengi waliokolewa kwa sababu aliwaambia habari za Injili ya Yesu Kristo. Aliyatumia maisha yake kwa kumtumikia Mungu

Siku moja kabla ya siku kuu ya Krismasi ya mwaka wa 1912, Lottie Moon alikuwa kwenye meli. Nayo ilikuwa kwenye bandari ya Kobe, Japan. Naye mmisheni mmoja mwuuguzi alimsindikiza. Naye alikuwa akimtunza Lottie Moon. Mara,

Kwa mara ya kwanza Lottie aliwacheka hao wasichana. Halafu asubuhi moja alifika kwenye mkutano wa maombi kuwaambia marafiki zake kwamba ametubu. Katika barua yake aliyowaandikia jamaa zake alisema: "Jana usiku nalienda kucheka kwenye ibada. Nilirudi chumbani mwangu ili niombe usiku kucha."

Lottie alikuwa ameshatubu kabisa moyoni mwake. Alikuwa ameshampokea Yesu kama Mwokozi wake.

**Sehemu ya Pili:** Mwito Wake

Lottie Moon akawa mwalimu wa shule. Kwa muda alifundisha katika shule ndogo ya kijiji chake. Dadaye mdogo alikuwa mmojawapo wa wanafunzi. Halafu baadaye alifundisha katika sehemu nyingine. Mchungaji wa kanisa la Kibatisti katika sehemu moja ya hizo aliyaandika maneno haya: "Miss Moon alikuwa akifundisha mahali hapa kwa muda wa miaka miwili. Kila mmoja alimpenda. Yeye alikuwa mwalimu mwaminifu katika Shule yetu ya Jumapili. Kila Jumapili alasiri, alikuwa akiwatafuta jamaa wenye shida na kuwafundisha neno la Mungu." Alikuwa akimtumikia Mungu kila mahali alipokuwa akiishi.

Alikuwa ameshasikia haja za watu wa China. Halafu jioni moja, baada ya mahubiri ya mmisheni, Lottie alikata shauri. Alimwambia mchungaji wake, "Nimejua kwa muda mrefu kuwa Mungu ananitaka niende katika nchi ya China. Sasa mimi ni tayari kwenda."

Lottie alianza kujitayarisha kwa safari yake ndefu ya kwenda China. Mnamo Agosti 18, 1873, Lottie aliondoka Amerika kwa meli kwenda katika nchi ambayo Mungu alimtaka amtumikie. Mnamo Oktoba 7, 1873, alifika mwisho wa safari yake.





ambacho Miriamu alikuwa akifanya wakati ambao Musa alikuwa katika hali ya kukua. Hakuna habari zake zilizoandikwa wakati ambao Musa na Haruni walikuwa wakimwomba Farao awakubalie wana wa Israeli kuondoka katika nchi ya Misri.

Tunaweza kusoma tena habari za Miriamu wakati ambapo wana wa Israeli walipokuwa wakiondoka kutoka katika nchi ya Misri. Wakati huo alikuwa na sehemu ya maana sana kati ya wanawake wa Kiebrania. Katika Kutoka 15:20 tunasoma maneno haya: "Na Miriamu, nabii mke..." Neno "Nabii mke" maana yake ni nabii mwanamke aliyeongozwa na roho wa Mungu kufundisha mapenzi yake Mungu. Tena litaweza kuwa na maana nyingine ya kuwa mke wa nabii. Walakini hata hivyo, hakuna mambo yaliyoandikwa kuonyesha ya kuwa Miriamu alipata kuolewa.

Ili ndipo wana wa Israeli waondoke kutoka katika nchi ya Misri, iliwalazimu kuvuka Bahari ya Shamu. Mfalme alikuwa ameshakubali kuwa watu wangeondoka lakini baadaye alibadilisha nia yake. Yeye pamoja na askari wake walianza kuwafuata. Naye Mungu aliwapatia njia ya kuokoka. Aliyafanya maji ya Bahari ya Shamu kutengana. Palikuwa na njia kavu kupita katikati ya Bahari. Nao wana wa Israeli walivuka kwa kupita hiyo njia kavu. Nao Wamisri waliwafuata kwa kupita Baharini. Walakini, walipokuwa katikati ya Bahari ya Shamu, wana wa Israeli walikuwa wamefika upande ule mwingine wakiwa salama salimini. Naye Mungu akayafanya maji ya Bahari ya Shamu kurudi mahali pake. Nao Wamisri walizama majini.

Hapa tunamwona Miriamu akiwa kama kiongozi kati ya wanawake wengine. Alitwaa tari (chombo cha muziki) mkononi mwake na kuwaongoza wale wanawake wengine kwa kuimba wimbo wa kumshukuru Mungu. Walimsifu Mungu kwa ajili ya kukombolewa kutoka kwa Wamisri. (Soma Kutoka 15:20-21).

**Sehemu ya Nne:** Dhambi Yake

Tena, wakati umepita kabla ya kusoma tena habari za Miriamu. Tena tunamwona Miriamu wakiwa na Haruni walipomnenea Musa ndugu yao. (Soma Hesabu 12:1-2). Hii hudhihirisha udhaifu katika tabia ya Miriamu. Hakupendezwa kuona kwamba Musa ameoa kutoka katika taifa lingine.

Naye Mungu aliyasikia mambo yale Miriamu na Haruni walikuwa wakimnenea Musa. Naye alihuzunika sana. Mungu alimwita Miriamu, Haruni na Musa kwenye hema ya kumwabudu Mungu. Mungu alinena nao kwa kumtetea Musa. Walipoondoka Miriamu alipatwa na ukoma. Hii ni kudhihirisha kuwa ndiye aliyekuwa chanzo cha huo mzozo. Naye Haruni aliuomba msamaha. Naye Miriamu alikaa nje ya kambi kwa muda wa siku saba. Naye Musa alimwomba Mungu ili amponye Miriamu. Miriamu aliweza kujifunza mambo mawili:

1. Mungu hapendezwi na watu wale ambao wanao chuki za kitaifa.
2. Mungu hapendezwi na watu wale ambao huwanenea wateule viongozi ambao huyafuata mapenzi yake.

Wakati wa mwisho ambao tunasoma habari za Miriamu ni katika Hesabu 20:1. Alifariki kabla ya wana wa Israeli kuingia katika Nchi ya Ahadi.

**Kiongozi:**

Leo tulipokuwa tukijifunza habari za Miriamu tumeshajifunza mambo fulani.

1. Mamaye alimfundisha kumwamini Mungu. Na sisi pia tungeweza kuwafundisha watoto wetu kumwamini Mungu.





Mpango wa Nne

## LOTTIE MOON

**Kuyasoma Maandiko:** Mathayo 9:36-38

**Kifungu cha Kukumbuka:**

*"Bwana ni mwema kwa hao wamngojeao, kwa hiyo nafsi imtafutayo."*

*Maombolezo 3:25*

**Kiongozi:**

Leo tutajifunza habari za mwanamke mmoja aliyemtumikia Mungu katika nchi ya China. Yeye alifanya mambo mengi ya ajabu kati ya wanawake wa nchi hiyo. Tutakuwa na wakati wa kujifunza kwa ufupi juu ya mwanamke huyu aitwaye Lottie Moon.

**Sehemu ya Kwanza:** Mwanzo wa Maisha Yake

Lottie Moon alizaliwa katika Amerika mnamo mwaka wa 1840, zaidi ya miaka iliyopita. Mama na babaye walikuwa na watoto wengine. Alipokuwa msichana mdogo, Lottie alifurahia kuyatenda mambo ya kujipendeza. Alikuwa mtoto mwenye furaha.

Shuleni Lottie alijifunza vizuri. Kwa kweli alikuwa akifaulu vizuri katika kila kitu. Yeye alikuwa kiongozi mzuri katika kila jambo. Mnamo mwaka wa 1859, aliingia katika shule ya masomo ya juu. Wakati huo shule yao ilikuwa na mikutano ya uhuisho. Lottie mwenyewe hakuwa Mkristo. Wakati wa ufufuo kundi la wasichana lilikuwa likikutana kwa ajili ya maombi. Katika mikutano yao hao wasichana walikuwa wakiomba sana kwa sababu ya kuongoka kwa Lottie Moon.

yalitumiwa kwa kuwabariki watu wengi duniani yapata zaidi ya miaka mia moja iliyopita. Hatuwezi kujua zaidi vile alivyomtumikia Mungu mpaka tutakapofika mbinguni na kufahamu wale watu aliowasaidia kumjua Mungu. Kwa sababu ya upofu wake hakutoa udhuru katika kumtumikia Mungu. Tusitoe udhuru katika huduma yake Mungu. Ebu na tujiweke mikononi mwa Mungu. Kisha naye atafanya nasi kama apendavyo.

ORODHA YA NYIMBO AMBAZO ZILIANDIKWA NA FANNY CROSBY.

(Hizi zinapatikana katika *Nyimbo za Sifa.*)

Nimekombolewa na Yesu, No. 82
Uniambie ya Yesu, No. 110
Atakaporudi tena Yesu, No. 115

Yesu Mkombozi wa Watu, No. 128
Mungu Mtukufu Aliye Bwana, No. 151
Ndiyo Dhamana, No. 154
Ni Wako Wewe, No. 161

(Hizi zinapatikana katika *Tenzi za Rohoni.*)

Yesu Akwita, No. 43
Waponyeni Watu, No. 60
Bwana U Sehemu Yangu, No. 116
Msifuni, Yesu Ndiye Mkombozi, No. 136





2. Alikuwa kiongozi katika kumshukuru Mungu kwa ajili ya ukombozi wa wana wa Israeli. Daima tunapaswa kumsifu Mungu kwa ajili ya ukombozi tulio nao katika Yesu.
3. Dhambi ikiwemo katika maisha ya mtu ye yote ni jambo baya. Ebu na tumwombe Mungu atupe ujasiri na imani ndani yake.

Ebu na tumwombe Mungu ili aondoe chuki ambazo zingeweza kuwa ndani ya mioyo yetu. Ebu na tumwombe Mungu atusaidie kuwaongoza marafiki zetu kwenda kwake.

Mpango wa Pili

## DEBORA

**Kuyasoma Maandiko:** Waamuzi 4:4-9

**Kifungu cha Kukumbuka:**

*" Mwamini Bwana Yesu, nawe utaokoka pamoja na nyumba yako."*

*Matendo 16:31*

**Kiongozi:**

Debora alikuwa akiishi miaka 1300 kabla ya kuzaliwa kwake Yesu. Yaani ni kusema ya kuwa alikuwa hai sasa yapata zaidi ya miaka 3,000. Zamani zile wanawake hasa hawakuwa na uongozi katika utawala wa mji au wa serikali. Hata hivyo, Debora alikuwa na nafasi katika uongozi. Katika cheo hiki cha uongozi, alikuwa akimhudumu Mungu.

**Sehemu ya Kwanza:** Nyakati za Maisha Yake

Nyakati ambazo Debora alikuwa akiishi zilikuwa zikijulikana kama "nyakati za waamuzi." Taifa la Israeli halikuwa na mfalme au kiongozi wa aina yo yote. Kwa hivyo shida zilitokea ndani na nje ya taifa. Mara kwa mara watu walikuwa wakimsahau Mungu na mambo yale waliyokuwa wameshajifunza hapo mbeleni. Walirudi kuabudu sanamu tena na wakatenda dhambi kwa njia nyingi. Naye Mungu alilikubalia taifa lingine kuwashinda Israeli vitani. Jambo hili liliwafanya wamkumbuke Mungu na kumwomba Yeye. Halafu Mungu alikuwa akimtuma mwamuzi kuwaongoza watu wapate kumrudia. Mwamuzi alipofariki, watu wengi walianza kumsahau Mungu tena. Walikuwa wakirudia njia za kutenda dhambi kwa mara nyingine.





**Sehemu ya Nne:** Utumishi Wake kwa Mungu

Baada ya Fanny kujitoa kwake Yesu, alianza kuziandika nyimbo nyingine nzuri kuhusu imani ya Kikristo. Wakati wa kufa kwake alikuwa ametunga mia ya nyimbo. Watu wengi walipata kumwamini Yesu kama Mwokozi wao kwa kuusikiliza ujumbe uliokuwa katika nyimbo hizo za Injili. Haijulikani kuwa ni elfu ngapi za Wakristo walioimarishwa imani yao ya Kikristo kwa njia ya nyimbo alizozitoa ulimwenguni.

Kulikuwa na njia nyingine ambazo Fanny Crosby alimtumikia Mungu nazo. Hata ingawa alikuwa kipofu, aliweza kuwafundisha vipofu wengine. Kwa sababu ya hekima yake kuu, watu wengi waliweza kutafuta mashauri yake. Aliweza kuelekeza maisha yao kwenye mapenzi ya Mungu. Pia alikuwa msemaji mashuhuri. Aliweza kueleza habari za pendo na neema ya Mungu katika sehemu nyingi, na kwa watu elfu nyingi.

**Kiongozi:**

Mkononi mwangu ninayo Biblia. Imetengenezwa kwa karatasi, na kitambaa, na maneno yaliyopigwa chapa. Hueleza habari za wokovu. Pia hueleza vile Mkristo awezavyo kuishi maisha yake kulingana na mapenzi ya Mungu. Hiyo karatasi na kitambaa zingeweza kutumiwa katika kuandika kitabu chenye mambo maovu. Tofauti kubwa iliyoko baina ya Biblia na kile kitabu kiovu haipatikani kutoka vitu vilivyotumiwa, lakini kutoka katika mtu yule aliyetumia vitu vile. Watu ambao wamempenda Mungu huweza kutumia karatasi na kitambaa na halafu chapa Biblia. Watu ambao huyatenda mapenzi ya Shetani huchukua karatasi na kitambaa halafu hutengeneza kitabu ambacho hutia sumu nia za watu.

Fanny Crosby aliyaweka maisha yake mikononi mwa Mungu. Alilipata jambo zuri kutoka maisha hayo. Maisha yake

**Sehemu ya Pili:** Mtunga Mashairi

Hatimaye aliweza kugunduliwa ya kuwa kulikuwa na kitu kimoja ambacho Fanny alitenda vizuri sana. Aliweza kuyatunga mashairi. Shairi lake la kwanza liliandikwa alipokuwa na umri wa miaka minane. Jirani na rafiki zake walimpa moyo wa kuendelea na kazi hii. Alipokua na kufikia msichana mkubwa, mashairi yake mengi yalikuwa yameshachapishwa. Pia aliandika maneno ya nyimbo zingine ambazo zilijulikana na zikapendwa na watu wengine wengi.

**Sehemu ya Tatu:** Kuongoka Kwake

Fanny alikuwa ameshajifunza mambo mengi kuhusu Biblia. Alihudhuria kanisani mara kwa mara. Hata hivyo hakuwa Mkristo mpaka alipotimiza umri wa miaka 31. Usiku mmoja aliota ndoto kwamba rafikiye alikuwa ameshafariki. Katika ndoto hiyo rafiki yake alimwambia Fanny atamkuta mbinguni. Jambo hili lilimfanya Fanny kuanza kufikiria sana juu ya mambo ya Mungu. Wimbo moja ulimsaidia kumfahamu Yesu. Aliyatoa maisha yake kwa Yesu alipoyasikia maneno haya:

*Lakini huzuni yote hailipi deni,*
*Najitoa kwako, Bwana, kama niwezavyo.*

(Hii ni beti ya nne ya wimbo ule, "Alisulibiwa Yesu", Nambari 104 katika *Nyimbo za Sifa.*)

Alifahamu ya kwamba Kristo peke yake ndiye ambaye angeweza kumwokoa. Hakuna lo lote ambalo angaliweza kulifanya ili aweze kuupata wokovu kwa nguvu zake mwenyewe. Lile ambalo angaliweza kulifanya ni kuyatoa maisha yake kwake Yesu ambaye alikufa kwa ajili yake. Alifanya hivyo kisha akapata amani na furaha.





Ulikuwa wakati mmoja wa nyakati hizi za shida ambazo mwamuzi wa kwanza mwanamke, yaani Debora, alitokea.

**Sehemu ya Pili:** Akiwa Hakimu

Biblia hunena habari za Debora kuwa alikuwa "Nabii mke." Tunakumbuka ya kuwa neno "nabii mke" maana yake ni "mwanamke aliyekuwa mjumbe wa Mungu." Alikuwa mke wa mtu mmoja aliyekuwa Lapidothi. Baraza la hukumu yake lilikuwa chini ya mtende katika nchi ya vilima vya Efraimu. Mara kwa mara waamuzi walikuwa wakisafiri katika nchi yote ya Israeli kwa kusikiliza kesi na kuziamua. Lakini Debora hakusafiri. Alikaa nyumbani. Watu walikuwa wakimwendea wakiwa na shida zao. Katika Waamuzi 4:5b twasoma, "---Wana wa Israeli wakakwea kwake, awaamue." Yeye alimwamini Mungu sana. Yeye aliweza kuwaongoza wengine kumwamini Mungu.

Jambo la maana sana katika maisha ya Debora ni kwamba alikuwa amechaguliwa na Mungu kuwa mwamuzi wa wakati huo. Mungu alimchagua ili ayajulishe mapenzi yake kwa watu wa Israeli, yaani wateule wake. Debora alikuwa mmoja ambaye Mungu alimtumia katika kuuleta ukombozi. Nao watu walimsikiliza Debora. Nao waliukubali uamuzi wake.

**Sehemu ya Tatu:** Wakati wa Shida za Taifa

Ikiwa kama adhabu ya maisha yao yenye dhambi, Mungu alimkubalia Yabini, mfalme wa Kanaani, kuwakamata watu wa Israeli. Yabini aliwatendea Waisraeli uovu mwingi. Alizitwaa ng'ombe zao. Aliharibu mashamba na nyumba zao. Shida na mateso zilijaa nchini.

Sisera alikuwa afisa wa jeshi la mfalme Yabini. Yeye alikuwa na askari wengi chini ya mamlaka yake. Pia alikuwa na magari ya farasi mia tisa yaliyoundwa kwa chuma. Magari hayo yalikuwa ya kupigana vita. Yalikuwa wazi upande wa nyuma. Na kila gari la farasi lilikuwa na mtu wa kuliendesha. Na kila moja lilikuwa na askari mwenye silaha za kupigana vita. Na kila gari

lilikuwa na mtu ambaye kazi yake ni kumlinda huyo askari. Hayo magari makubwa ya farasi yangeweza kutumiwa tu katika nchi tambarare. Hayakuwa na faida katika nchi za milima.

Watu wa Israeli walimwogopa Sisera pamoja na askari wake. Naye Debora aliagizia mtu mmoja aitwaye Baraka aje amsaidie. Naye Baraka alifika na akayasikia maneno ya Mungu kutoka kwa Debora. (Soma amri hii kutoka katika Waamuzi 4:6-7). Mungu alimwamuru Baraka kuchukua watu elfu kumi (10,000) waende kuelekea kwenye mlima. Mungu alikuwa na mpango wa ukombozi. Kulikuwa na ahadi ya ushindi.

Baraka alifahamu ya kuwa Mungu alikuwa akimwongoza Debora. Pia alijua ya kuwa yeye mwenyewe alihitaji mashauri ya Debora. Kwa hivyo, alijibu, "Kama utakwenda pamoja nami, ndipo nitakwenda; bali kama huendi pamoja nami, mimi siendi" (Waamuzi 4:8). Naye Debora alijibu kwa kusema ya kuwa angekwenda pamoja naye. Naye akamwambia Baraka ya kuwa hangepata heshima ya ushindi. Akasema, "...maana Bwana atamwuza Sisera katika mkono wa mwanamke." (Soma Waamuzi 4:9).

**Sehemu ya Nne:** Ushindi

Baraka alikusanya watu pamoja kama vile Debora alikuwa amesema. Neno lilimfikia Sisera kwamba Baraka pamoja na majeshi yake wamekwenda mlima wa Tabori. Naye Sisera alianza kujitayarisha kupigana vita.

Wakati ulipowadia, Debora alimwambia Baraka, "Haya! inuka, maana siku hii ndiyo siku ambayo Bwana amemtia Sisera katika mkono wako. Je! Bwana hakutoka atangulie mbele yako?" (Waamuzi 4:14).





Mpango wa Tatu

## FANNY CROSBY

**Kuyasoma Maandiko:** Zaburi 101:1-3

**Kifungu cha Kukumbuka:**

*"Nitayainua macho yangu niitazame milima; msaada wangu utatoka wapi?"*

*Zaburi 121:1*

**Kiongozi:**

Leo tutajifunza habari za mwanamke aliyezaliwa yapata sasa miaka 150 iliyopita. Jina lake lilikuwa Fanny Crosby. Alipokuwa na umri wa wiki sita, macho yake yaliambukizwa na ugonjwa. Na baada ya muda mfupi alipatwa na upofu. Pengine ungeuliza, "Awezaje mwanamke ambaye aliupata upofu tangu utoto wake kumtumikia Mungu?" Jambo hili ni la kushangaza. Ni ajabu kujua vile Mungu alivyomtumia mwanamke huyu.

**Sehemu ya Kwanza:** Wakati wa Utoto Wake

Fanny Crosby alikataa kuketi chini na kuukubalia upofu uyaharibu maisha yake. Yeye alikuwa msichana mwenye furaha ambaye alipendezwa na kila jambo lililomzunguka. Hata aliweza kucheza michezo fulani na wale watoto wengine. Nyanya yake alikuwa msaada mkubwa kwake. Yeye aliketi kwa muda mrefu kwa kumsimulia hadithi huyo mjukuu wake. Nyanya yake ndiye aliweza kuuona uzuri wa dunia ya Mungu. Aliweza kuyaeleza mambo yote kwa Fanny. Hakika wakati huo, Fanny alikuwa hawezi kujisomea Biblia. Nyanya yake alimsaidia kujifunza vifungu kutoka Biblia. Baadaye aliweza kujifunza kusoma kwa kuviweka vidole vyake juu ya herufi zilizoinuliwa, ili aweze kuzipapasa kwa vidole vyake.

**Kiongozi:**

Tumeshajifunza ya kuwa Prisila pamoja na mumewe walikuwa wakimtumikia Mungu wakiwa pamoja. Nyumba yao ilikuwa mahali ambapo watu walienda kujifunza mengi kuhusu Kristo. Prisila na Akila walijifunza mambo mengi kutoka kwake Paulo wakati alipokuwa akikaa nao nyumbani kwao. Nao waliweza kuyafundisha mambo haya kwa Apolo walipokuwa katika Efeso.

Ni jambo la maana sana siku hizi kwa mume na mke kumtumikia Mungu wakiwa pamoja. Pia ni jambo jema wakati

Ni jambo la maana sana siku hizi kwa mume na mke kumtumikia Mungu wakiwa pamoja. Pia ni jambo jema wakati rafiki zetu wanapokuja nyumbani kwetu wakitaka kujifunza mengi kuhusu Mungu. Tunapaswa kutumia nyumba zetu kama mahali pa kuwashuhudia watu wengine. Na tuombe kwamba Mungu angetutumia pamoja na nyumba zetu katika njia hii.





Ushindi ulikuwa wao. Mungu aliituma mvua kubwa juu ya jeshi la Sisera. Askari walitoroka walipomwona Baraka na watu wake. Magari ya farasi hayangeweza kutembea kwa sababu ya matope na maji. Sisera akashuka kutoka katika gari lake akakimbia. Naye alifika kwenye hema ya mtu ambaye alifikiria kuwa ni rafiki. Naye mwanamke alimpa chakula na mahali pa kupumzika. Na alipokuwa usingizini, yule mwanamke aliyeitwa Yaeli alimwua Sisera. Hatimaye Baraka alifika kwenye hiyo hema. Naye yule mwanamke alitoka kwenda kumlaki Baraka akimwambia, "Njoo, nami nitakuonyesha yule unayemtafuta" (Waamuzi 4:22b). Ilikuwa kama vile Debora alikuwa ameshatabiri. (Soma Waamuzi 4:9). Mungu akampatia ushindi Debora, Baraka na watu wa Israeli.

Debora na Baraka waliimba wimbo wa kumshukuru Mungu. "Kwa sababu wakuu walitangulia katika Israeli, kwa sababu watu walijitoa nafsi zao kwa hiari yao, Mhimidini Bwana" (Waamuzi 5:2). Wimbo huu hupatikana katika mlango wa tano wa kitabu cha Waamuzi. Katika wimbo huu wote tutaweza kuona vile Debora alivyomwamini Mungu. Pia tutaweza kujua ya kuwa alikuwa na shukurani kwa ajili ya ushindi. Sasa watu wake walikuwa na uhuru. Hawakuwa tena watumwa wa taifa lingine. Wimbo huu wa kusifu umefuatwa na maneno: "Nayo nchi ikastarehe miaka arobaini" (Waamuzi 5:31b).

**Kiongozi:**

Leo tunafanana na watu wa nyakati za Debora. Twamsahau Mungu na hata zile baraka alizotubariki nazo. Somo hili la leo linapaswa kutukumbusha ya kuwa ni dhambi kumsahau Mungu. Tunamsahau Mungu tunapoendelea kukosa kuhudhuria ibada kanisani pamoja na watu wengine. Ebu na tumwombe Mungu ili atusaidie tukumbuke baraka zile ambazo ametupa.

Tukiwa kama wanawake, tutaweza kumtumikia Mungu kama vile Debora alivyomtumikia. Imani yake kwa Mungu ilimsaidia Baraka. Pia iliwasaidia askari wa Israeli kumwamini Mungu zaidi. Kama imani yetu kwa Mungu ni kubwa sana, basi tutawaongoza wengine kumwamini yeye. Ebu na tumwombe Mungu atusaidie kuwaongoza wengine kwake yeye.





**Sehemu ya Tatu:** Katika Efeso

Walipofika Efeso, Paulo aliingia katika Sinagogi na akahojiana na Wayahudi. (Tazama Matendo 18:19). Papo hapo wakimwomba Paulo akae nao kwa muda mwingi zaidi. Lakini hakuweza kufanya hivyo. Yeye alisema, "Nitarejea kwenu tena, Mungu akinijalia" (Matendo 18:21b). Alipoondoka Efeso, aliwaacha Prisila na Akila huko. Nao walikuwa viongozi wa kanisa la Efeso. Paulo aliporudi Efeso tena alikuta kundi la wenye kuamini.

Prisila alimtumikia Mungu sana katika Efeso. Yeye pamoja na mumewe walimkuta mtu mmoja jina lake Apolo. Apolo alikuwa mtu wa elimu kutoka katika Iskanderia, nchi ya Misri. Mtu huyu alifahamu sana mafundisho ya Agano la Kale. Pia alijua mafundisho juu ya Yohana Mbatizaji kuhusu Yesu. Lakini hakujua juu ya kufa na kufufuka kwa Yesu.

**Sehemu ya Nne:** Kumfundisha Apolo

Naye Apolo alianza kufundisha na kuhubiri katika Sinagogi. Wakati Prisila na Akila walipoyasikia mafundisho yake, walijua ya kuwa hakujua mambo yote kuhusu Yesu. Kwa hivyo, "Wakamchukua kwao, wakamweleza njia ya Bwana kwa usahihi" (Matendo 18:26b). Yale ambayo Apolo alikuwa ameshayajua yalikuwa kweli. Lakini alikuwa hajajua mengi kuhusu maisha ya Yesu.

Mafundisho ya maana ambayo Apolo alipata kuyapokea, aliyapata kutoka katika nyumba ya Prisila na Akila. Utumishi mkubwa ambao Prisila na Akila walipata kumtendea Mungu ulikuwa ndio huo wa kumfundisha Apolo. Prisila alimtaka awe mtu aliyeijua vizuri Injili yote.

Nyumbani kwake kulikuwa mahali pa kukutanika watu wale waliopenda kujua zaidi habari za imani ya Kikristo. Yeye pamoja na Akila walikuwa wakiishi wakati ambao maisha yalikuwa magumu kwa Wakristo. Wakristo wa siku zile walipata mateso mengi. Hata wengine waliuawa kwa ajili ya kumwamini Mungu. Prisila alipenda kujinyima kwa ajili ya kueneza Injili. Hakuogopa wakati wa hatari.

Hili ni jambo ambalo Wakristo wa siku hizi linawabidi kushindania. Tunapowaambia wengine habari za wokovu katika Yesu Kristo hatuteswi wala kuuawa. Lakini watu wengi huogopa kusema habari za Kristo kwa marafiki zao.

**Sehemu ya Pili:** Katika Korintho

Prisila na mumewe Akila walikuwa wakiishi katika mji wa Rumi. Mambo yaliyotukia katika mji huo yaliwalazimisha Wayahudi wote kuuhama mji wa Rumi. (Soma Matendo 18:2). Baada ya kuondoka Rumi Prisila na Akila walihamia katika mji wa Korintho. Katika mji huu Paulo alikutana na watu hawa wawili.

Paulo alikuwa mmisheni wa kwanza. Yeye alisafiri sana na aliweza kuzuru sehemu nyingi. Wakati alipokuwa katika safari yake ya pili ya umisheni, alifika katika Korintho. Yeye pia alikuwa ameshajifunza kushona hema. Kwa hivyo alipokutana na Prisila wakiwa na mumewe, alikaa nao. Alikaa nyumbani kwao kwa muda wa mwaka mmoja na miezi sita. Katika Matendo 18:11 tumeambiwa ya kuwa Paulo alikuwa akifundisha kati ya watu neno la Mungu. Wakati Paulo alikaa kwao, Prisila na Akila walijifunza mambo mengi kuhusu Yesu.

Paulo alipoondoka kutoka katika Korintho, Prisila na Akila walienda pamoja naye. Nao wakafika katika mji wa Efeso.





Mpango wa Tatu

## MJANE WA SAREPTA

**Kuyasoma Maandiko:** 1 Wafalme 17:12-13, 24

**Kifungu cha Kukumbuka:**

*"Na Mungu wangu atawajazeni kila mnachokihitaji kwa kadiri ya utajiri wake, katika utukufu, ndani ya Kristo Yesu."*
*Wafilipi 4:19*

**Kiongozi:**

Katika somo letu la leo hatuelezwi juu ya jina la mwanamke aliyemhudumu Mungu. Yeye alijulikana kwa jina la kijiji alichokiishi. Mwanamke huyu alikuwa ameshaolewa. Na mumewe alikuwa ameshafariki. Naye alikuwa na mwana mmoja. Leo tutajifunza vile mwanamke wa Sarepta alivyojifunza jinsi ya kumwamini Mungu.

**Sehemu ya Kwanza:** Kukutana na Nabii Eliya

Kwa muda wa miaka miwili na nusu kulikuwa na ukosefu wa mvua katika nchi ile ambayo yule mjane alikuwa akiishi. Kabla ya ukavu, Eliya aliende akasimama mbele za mfalme Ahabu. Alimwambia mfalme ya kuwa Mungu angetuma ukavu. Hii ilikuwa ni kama adhabu kwa ajili ya dhambi za watu. Kisha Mungu alimtuma yule nabii kwenda kuishi karibu na kijito cha Kerithi. Na pale nabii angeyapata maji ya kunywa. Naye Mungu angemtumia chakula. Punde kwa punde kile kijito kilikauka. Naye Mungu alimwambia Eliya, "Ondoka, uende Sarepta, ulio mji wa Sidoni, ukae huko. Tazama, nimemwagiza mwanamke mjane wa huko akulishe" (1 Wafalme 17:9).

Katika mji wa Sarepta yule mjane pamoja na mwanawe walikuwa wenye njaa. Ndani ya nyumba yake alikuwa tu na

konzi ya unga na mafuta kidogo yaliyobaki. Pengine alikuwa hana tumaini kwa sababu ya ukosefu wa chakula. Alikuwa ametoka nje kwenda kuokota kuni.

Alipokuwa akiziokota kuni, Eliya alimwona. Mungu alikuwa ameshamtuma Eliya kwenda kwa mwanamke huyo. Imani yake Eliya ilijaribiwa. Alikuwa amejifunza ya kuwa Mungu aliweza kumtunza. Sasa aliweza kumhakikishia mjane ya kuwa Mungu angemtunza. Eliya alimwambia yule mjane: "Niletee, nakuomba, maji kidogo chomboni nipate kunywa" (1 Wafalme 17:10b). Naye alianza kwenda kuyaleta, Halafu Eliya akasema, "Niletee, nakuomba, kipande cha mkate mkononi mwako" (1 Wafalme 17:11).

**Sehemu ya Pili:** Imani ya Mjane Ilipojaribiwa

Naye yule mjane alijibu ya kuwa hakuwa na mkate. Naye alimwambia nabii ya kuwa palikuwa pamebaki chakula na mafuta kidogo. Mpango wake ulikuwa kutayarisha moto na kupika hicho chakula kidogo. Halafu yeye pamoja na mwanawe wangekufa.

Naye Eliya alimwambia, "Usiogope; enenda ukafanye kama ulivyosema; lakini unifanyie kwanza mkate mdogo ukaniletee; kisha ujifanyie nafsi yako na mwanao" (1 Wafalme 17:13). Kumbuka ya kuwa mwanamke huyu na mwanawe walikuwa wenye njaa. Je! kama ungesimama mahali pake ungefanya nini? Katika 1 Wafalme 17:14 Eliya aliyanena maneno ya ahadi kwa huyo mjane. (Soma kifungu hiki). Huko ni kujaribiwa kwa imani ya mama na mwana wenye njaa. Ni ahadi ya ajabu.

**Sehemu ya Tatu:** Imani ya Mjane Yaimarishwa

Mjane aliyasikiliza maneno ya Eliya. Eliya alisema ya kuwa ni lazima apewe chakula hicho na mafuta hayo kidogo. Naye huyo mjane alitengeneza mkate. Naye alitumia chakula





Mpango wa Pili

## PRISILA

**Kuyasoma Maandiko:** Matendo 18:24-28

**Kifungu cha Kukumbuka:**

*"Jitahidi kujionyesha kuwa umekubaliwa na Mungu, mtenda kazi asiye na sababu ya kutahayari, ukitumia kwa halali neno la kweli."*

*2 Timotheo 2:15*

**Kiongozi:**

Prisila alikuwa mwanamke mwenye msaada sana katika kanisa la Agano Jipya. Jina la mumewe lilikuwa Akila. Walikuwa wakisaidiana katika kumhudumia Mungu. Leo tutajifunza njia ambazo walimhudumia Mungu katika miaka ya kwanza ya kulianzisha kanisa.

**Sehemu ya Kwanza:** Tabia Zake

Prisila pamoja na mumewe walikuwa wakifanya kazi ya kushona hema. Walifanya kazi wakiwa pamoja nyumbani kwao. Prisila pia alikuwa akiwatumikia wale wa nyumbani kwake. Ingawaje alizitenda kazi hizi, alipata nafasi ya kujifunza Injili ya Yesu Kristo kwa njia nzuri. Hakuwa mtu mwenye elimu nyingi kutoka katika shule au kutoka katika chuo kikuu. Lakini hata hivyo aliyajua mambo ya imani ya Kikristo. Aliyajua mambo hayo kwa akili na kwa moyo.

Tunaposoma habari za Prisila katika Agano Jipya tunaona mambo mazuri kuhusu tabia zake. Hakujifanya kuwa wa mbele. Hakujifanya kuwa mkubwa wa watu wale wengine. Yeye alifuata mafundisho ya Paulo: "Enyi wake, watiini waume zenu kama kumtii Bwana wetu" (Waefeso 5:22).

MACHI

Mpango wa Kwanza

## JUMA LA MAOMBI

## 1982

Katika kitabu hiki hakutakuwa na mpango wa kawaida kwa wiki hii. Kuna kijitabu kingine ambacho mtapata kwa njia ya Posta.

Sadaka za juma hili za Wanawake Wabatisti wa Kenya zitumwe kwa:-

Bi. Joan Carter
Baptist Publications House
P.O. Box 30370
Nairobi, Kenya

Sadaka za juma hili za Wanawake Wabatisti wa Tanzania zitumwe kwa:-

Bi. David Whitson
S.L.P. 1099
Bukoba, Tanzania





kilichokuwa ndani ya pipa. Alitumia mafuta kutoka katika chupa. Ni tendo la imani. Kwa ajili ya kutii amri ya nabii, alifahamu utimilivu wa ahadi.

Wakati wa ukavu, alishuhudia mwuujiza kila siku. Katika 1 Wafalme 17:15b tunasoma, "Yeye mwenyewe, na Eliya, na nyumba yake, wakala siku nyingi."

Mahali hapa, tunajifunza mambo mawili kutoka katika maisha ya mjane. Kwanza, alitamani kutoa vyote alivyokuwa navyo kwa nabii. Pili, aliamini maneno ya nabii aliposema, "Chakula hakitapungua." Imani yake ilijaribiwa. Pia imani yake iliimarishwa kwa sababu ya kujaribiwa.

**Sehemu ya Nne:** Mjane na mauti

Baada ya mambo haya kutukia, imani ya mjane ilijaribiwa tena. Wakati huu mwanaye alikuwa mgonjwa sana. Alikuwa mgonjwa sana hata akafariki. Imani ya mjane haikuwa na nguvu kuweza kustahimili shida hii. Alianza kumtukana yule nabii. (Soma maneno ya 1 Wafalme 17:18).

Eliya alimwamuru yule mwanamke akisema, "Nipe Mwanao." Aliutwaa mwili wa yule mtoto kutoka kwa mamaye. Kisha alienda peke yake akiwa na ule mwili katika chumba kingine. Akiwa peke yake ndani alimwomba Mungu. Aliunyosha mwili wake juu ya mwili wa yule kijana safari tatu. "Akamwomba Bwana, akanena, "Ee Bwana, Mungu wangu," nakusihi, roho ya mtoto huyu imrudie ndani yake" (1 Wafalme 17:21b). Mungu alilisikia ombi la Eliya. Mungu aliurudisha tena uhai wa huyo kijana. Eliya akamrudisha yule mtoto kwa mamaye. Naye alisema, "Tazama, mwanao yu hai" (1 Wafalme 17:23b).

Mwujiza mwingine ulitukia katika nyumba ya yule mjane. Nabii alidhihirisha nguvu zake Mungu za kuponya na kumfufua mtu kutoka kwa wafu. Akiwa na imani kuu yule mwanamke

alimwambia Eliya, "Sasa najua ya kuwa wewe ndiwe mtu wa Mungu, ya kuwa neno la Bwana kinywani mwako ni kweli" (1 Wafalme 17:24).

**Kiongozi:**

Huyu mjane wa Sarepta alikuwa ameshapoteza tumaini lote katika maisha wakati Eliya alipokutana naye. Halafu Eliya alimwambia Neno la Mungu. Neno hili lilikuwa la kujaribu imani yake. Hata hivyo, aliyaamini maneno ya Mungu. Alimtunza Eliya. Kwa kufanya hivyo haja zake zilitimizwa. Hata wakati wa kufa kwa mwanaye aliye wa pekee Mungu aliweza kumtimizia hàja zake.

Ni lazima siku hizi tumwamini Mungu kabisa. Ni lazima tumtumikie kwa imani kama vile huyo mjane alivyofanya hapo kale. Siku hizi Mungu yuko tayari kutimiza haja zetu. Hukupatia kila kitu tunachokitamani. Kifungu chetu cha kukumbuka cha siku hii ya leo kinatuambia ya kuwa Mungu atutimizia *haja* zetu wala siyo *tamaa* zetu.

Ebu na tumwombe Mungu ili atusaidie ili ndipo tumtumikie tukiwa na imani kuu.





Yeye alimpenda Yesu zaidi ya mambo yote. Pia ni lazima tumfanye Kristo kuwa wa kwanza ndani ya maisha yetu. Yesu alisema ya kuwa, ikiwa tunapenda vitu vyo vyote zaidi ya vile tumpendavyo, basi hatufai kuitwa watu wake (Soma Mathayo 10:37-39).

Mariamu wa pili ambaye tumejifunza habari zake, anakumbukwa kama mama yake Yohana ambaye jina lake la pili ni Marko. Siku hizi tunalifahamu jina lake kuwa ni "Marko." Yeye ndiye aliyeandika kitabu cha Injili ya Marko.

Mariamu alimtumikia Mungu akiwa nyumbani kwake. Wakristo walikuwa wakikutana humo kwa ajili ya maombi na ushirika. Ulikuwa ushuhuda wa ajabu kwa wale waliokuwa wakiishi karibu naye. Je! siku hizi nyumba zetu ni ushuhuda mwema kwa ajili ya Kristo na pendo lake kwa watu wote?

**Kiongozi:**

Tumejifunza tena vile tuwezavyo kumtumikia Mungu kwa njia iliyo bora. Ni jambo la maana sana kuwafundisha watoto wetu jinsi tumpendavyo Mungu. Wangeweza kujifunza kwa njia nyingine ipi? Ikiwa tunasema tu kwa maneno ya kwamba tunampenda Mungu, watoto wetu watajua ya kuwa hatumpendi Mungu zaidi ya mambo yale mengine yote.

Kwa sababu sisi tu Wakristo, nyumba zinapaswa kuwa ushuhuda mwema kwa jirani zetu. Tena ni jambo la maana sana kuonyesha kwa maisha yetu ya kwamba tunamtumikia Mungu.

Ebu na tumwombe Mungu ili atupe nguvu na hekima tunapomtumikia tukiwa kwetu nyumbani. Tumwuulize jinsi nyumba zetu zingeweza kutumiwa kwa ajili yake.

Tunaliona jina lake katika kifungu kimoja tu cha Biblia. (Soma Matendo 12:12). Kwa sababu ya kifungu hiki, Mariamu amejulikana kwetu kama mmoja wapo wa wanawake wakuu katika Agano Jipya. Katika kifungu hiki kimoja tunayaona maneno haya, habari za mkutano katika nyumba ya Mariamu. "Watu wengi walikuwa wamekutana humo wakiomba." Ni jambo kuu kuongea habari za nyumba ya mtu. Jambo hili lilitukia miaka kumi au kumi na miwili baada ya Yesu kupaa kwenda mbinguni.

Naye Petro alikuwa amefungwa gerezani kwa sababu ya kumwamini Kristo. Mfalme alikuwa na mpango wa kumwua Petro. Walakini, malaika wa Bwana alimtoa Petro kutoka gerezani. Huu ulikuwa mwujiza. Wakati Petro alipofahamu ya kuwa ameokolewa kutoka katika mkono wa mfalme, alienda mpaka kwenye nyumba ya Mariamu.

Nao wale Wakristo waliokuwa Yerusalemu walihangaika sana kuhusu Petro. Watu wengi walikuwa wamekutana nyumbani mwa Mariamu. Walikuwa wakimwombea Petro. Hatujui, pengine walikuwa wameshakutana humo mara nyingi. Tunadhani ya kuwa nyumba yake ilikuwa mahali pa mikutano kama huu. Katika siku zile, mtu mwenye ujasiri tu ndiye ambaye angekubali nyumba yake kutumiwa kwa maombi. Ilikuwa hatari mtu kujulikana kuwa ni Mkristo.

Siku hizi tukiwa kama Wakristo, nyumba zetu zinapaswa kuwa mahali ambapo Wakristo huweza kukutana kwa ajili ya maombi na kujifunza Biblia.

**Sehemu ya Nne:** Mafundisho ya Leo

Mariamu wa kwanza ambaye tumejifunza habari zake alijulikana kama "Mariamu mama yao Yakobo na Yusufu." Hakika aliwafundisha wanawe habari za Mungu. Ni jambo la maana sana siku hizi kuwafundisha watoto wetu mambo ya Mungu.





Mpango wa Nne

## MWANAMKE WA SHUNEMU

**Kuyasoma Maandiko:** 2 Wafalme 4:8-10

**Kifungu cha Kukumbuka:**

*"--- kwa wanadamu hilo haliwezekani; bali kwa Mungu yote yawezekana."*

*Mathayo 19:26*

**Kiongozi:**

Leo tutajifunza habari za mwanamke mwingine aliyehudumia Mungu. Tena hatulijui jina la huyo mwanamke. Biblia humwita "Mwanamke mwenye cheo." Pia Biblia humwita "Mwanamke Mshunami" au mtu wa kutoka Shunemu.

Ukweli kwamba aliitwa "Mwanamke mwenye cheo," pengine ni kwa sababu alikuwa mtu mwenye mali. Au pengine alikuwa na mvuto kwa watu wengine. Tunapoendelea kujifunza juu ya mwanamke huyu tutaona ya kuwa alikuwa mwenye cheo katika njia zingine. Alikuwa mkuu katika hekima na shauku katika kazi ya Mungu. Alikuwa mkuu katika imani yake kwake Mungu. Yeye alikuwa mkuu katika kukaa kimya wakati wa kifo.

**Sehemu ya Kwanza:** Pendo Lake kwa Kazi ya Mungu

Mshunami alikuwa akiishi karibu na barabara inayotoka Nazareti kwenda Yerusalemu. Mara kwa mara nabii Elisha alikuwa akipitia njia ile. Siku moja mwanamke huyu alishiriki chakula chake pamoja na Elisha. Ikawa kila alipopita njia ile, huingia kula chakula. (Soma 2 Wafalme 4:8).

Mwishowe yule mwanamke alimwambia mumewe, "Tazama mimi naona ya kuwa mtu huyu apitaye kwetu mara

kwa mara ni mtu mtakatifu wa Mungu. Nakuomba, tumfanyie chumba kidogo ukutani; na ndani yake tumwekee kitanda, na meza, na kiti, na kinara cha taa; na itakuwa, atujiapo, ataingia humo." (Soma 2 Wafalme 4:9-10). Kwa hivyo walimjengea chumba ukutani mwa nyumba yao.

Hii hutueleza jinsi alivyojishughulisha juu ya starehe ya Elisha. Elisha alikuwa nabii mzuri. Naye mwanamke huyu alimpenda Mungu pamoja na kazi yake. Alikuwa mwenye hekima kwa kutambua ya kuwa Elisha alikuwa mtu wa Mungu.

**Sehemu ya Pili:** Imani yake kwake Mungu

Siku moja wakati Elisha alipokuwa ndani ya nyumba ya mwanamke huyu alimtuma mtumishi wake kwenda kumwita. Naye alikuja akasimama mbele zake Elisha. Naye, Elisha alisema, "Tazama, wewe umetutunza sana namna hii, utendwe nini basi? Je! uombewe neno kwa mfalme, au kwa amiri wa Jeshi?" (Soma 2 Wafalme 4:13). Akasema ya kuwa hakutafuta upendeleo.

Naye Elisha alizungumza na Gehazi mtumishi wake, juu ya jambo hili. Naye Gehazi alimkumbusha huyo nabii ya kuwa huyo mwanamke hakuwa na mwana. Tena alimwambia ya kuwa mumewe alikuwa mzee.

Elisha alimwita huyo mwanamke tena. Naye alikuja akasimama mbele yake. Elisha alisema, "Panapo wakati huu mwakani, utamkumbatia mwana" (2 Wafalme 4:16). Wakati ulitimia na alimzaa mwana, wakati ule ule ambao Elisha alimwambia.

Miaka mingi ilipita, pengine miaka kumi au kumi na miwili. Biblia imetuambia ya kuwa yule kijana alienda shambani pamoja na babaye.





**Sehemu ya Pili:** Njia Ambazo Alimtumikia Yesu

Katika sehemu ya kwanza ya kazi yake Yesu, hatusomi habari za huyu Mariamu. Agano Jipya limetuambia habari zake katika mwisho wa maisha ya Yesu hapa ulimwenguni.

Mariamu huyo alikuwapo wakati wa kusulibiwa kwake Yesu msalabani. Yeye pamoja na watu wengine walimfuata Yesu kutoka katika Galilaya. Wakati huo Mariamu alikuwa akijishughulisha katika kumtumikia Yesu (Soma Mathayo 27:55-56).

Wakati mwili wa Yesu ulipotolewa msalabani Mariamu alikuwako. Alimfuata Yusufu wa Arimathaya mpaka kaburini. Naye angekuwa ametazama wakati mwili wake ulipowekwa kaburini. Baada ya kaburi kufungwa, kila mmoja alienda zake isipokuwa Mariamu, mama yao Yakobo na Yusufu, na Mariamu Magdalene. Hawa wawili hawakupenda kutoka kaburini.

Tutaweza tu kufikiria juu ya huzuni ambayo ilikuwa moyoni mwa Mariamu wakati wa Yesu kusulibiwa msalabani mpaka wakati wa kufufuka kwake. Pengine watu wengi waliulizana, "Je! imekwisha? Kutatukia nini sasa?"

Huyu Mariamu alikuwa mmoja wa wanawake waliokwenda kaburini kwa Yesu. "Hata sabato ilipokuwa, ikipambazuka siku ya kwanza ya juma, Mariamu Magdalene, na Mariamu yule wa pili, walikwenda kulitazama kaburi" (Mathayo 28:1). Katika somo letu la juma lililopita tulijifunza habari za mambo yaliyotukia katika kufufuka kwa Yesu. Mariamu alikuwa na furaha sana alipojua ya kuwa Yesu amefufuka. "Amefufuka kutoka kwa wafu." Yeye pia, alikuwa na habari njema za kuwaambia watu wengine.

**Sehemu ya Tatu:** Mama yake Yohana Marko

Mariamu mwingine ambaye tutajifunza habari zake ni Mariamu mamaye Yohana ambaye jina lake la pili ni Marko.

FEBRUARI

Mpango wa Nne

## WANAWAKE WAWILI WAITWAO MARIAMU

**Kuyasoma Maandiko:** Mathayo 27:54-56

**Kifungu cha Kukumbuka:**

*"Nanyi enendeni upesi, mkawaambie wanafunzi wake, Amefufuka katika wafu..."*

*Mathayo 28:7a*

**Kiongozi:**

Jina "Mariamu" limetumiwa mara nyingi zaidi ya jina lingine la mwanamke katika Agano Jipya. Kuna wanawake sita walio tofauti katika Agano Jipya wanaoitwa "Mariamu." Katika maisha ya kila mmoja wa wanawake hao tutaweza kuona jinsi walivyokuwa na upendo na uaminifu kwake Mungu. Leo tutajifunza habari za wanawake wawili kati ya hao. Wa kwanza ndiye Mariamu mama yao Yakobo na Yusufu. Na yule mwingine ni Mariamu mama yake Yohana ambaye jina lake la pili ni Marko.

**Sehemu ya Kwanza:** Mamaye Yakobo na Yusufu

Mariamu wa kwanza ambaye tutajifunza habari zake anajulikana kama mama yake Yakobo na Yusufu. Ametajwa jina lake katika Injili ya Mathayo, Marko na Luka. Katika Injili ya Yohana ameitwa "Mke wa Klopa." Mwanawe Yakobo alikuwa mmoja wa wale wanafunzi kumi na wawili wa Yesu. Husema ya kuwa Yakobo alihubiri katika nchi ya Palestina na katika nchi ya Misri. Hao wana wawili wa Mariamu walisaidia katika kuanzisha kanisa la kwanza. Hakika mwanamke huyu alimpenda Mungu zaidi ya mambo mengine yote. Kwa kweli aliwafundisha wanawe juu ya pendo hili.





Ulikuwa wakati wa kuvuna mavuno. Kulikuwa na joto na ukavu. Mtoto alikuwa hajakaa sana kwenye joto aliposema kwa babaye, "Kichwa changu! kichwa changu!" (2 Wafalme 4:19a). Naye babaye alimwambia mtu mwingine aliyekuwa akimsaidia kufanya kazi, "Mchukue kwa mama yake" (2 Wafalme 4:19b). Naye mama alimchukua yule mtoto mkononi mwake mpaka alasiri. Kisha akafa. Ingawaje mwanawe wa pekee alikufa, aliendelea katika kumwamini Mungu.

**Sehemu ya Tatu:** Ukimya Wake Wakati wa Kifo

Kwa haraka yule mwanamke alimchukua mwanaye akampeleka katika chumba cha yule nabii. Aliuweka mwili wa mwanaye juu kitandani na akaondoka. Mwanamke yule hakumnung'unikia mumewe. Hakuomboleza wala kulia. Alituma neno kwa mumewe akisema: "Tafadhali, uniletee mmoja wa wale watumishi, na punda mmoja, ili nimwendee mtu wa Mungu kwa haraka nikarudi tena" (2 Wafalme 4:22). Hakulalamika kwa mumewe.

Yeye pamoja na mtumishi wao walijitayarisha mara moja. Walisafiri wote pamoja kuelekea mlima wa Karmeli. Walipoukaribia, Elisha aliwaona. Naye alimtuma Gehazi kwenda kumwuliza, "Hujambo? Mume wako hajambo? Mtoto hajambo?" (2 Wafalme 4:26). Naye alijibu, "Hawajambo." Yeye alikuwa kimya kuhusu kifo cha mtoto.

Alikimbia kuelekea kwa yule nabii na alianguka miguuni pake. Elisha alifahamu ya kuwa roho yake yule mwanamke ina uchungu. Hatimaye aliweza kufahamu ugumu wa jambo hilo. Naye nabii alimwambia Gehazi, "Jikaze viuno, ukachukue fimbo yangu mkononi mwako, ukaende........Ukaweke fimbo yangu juu ya uso wa mtoto" (2 Wafalme 4:29). Halafu Elisha aliondoka na kumfuata yule mwanamke Mshunami.

Walipofika nyumbani kwa yule mwanamke, mtoto alikuwa angali amekufa. Elisha peke yake ndiye aliyeingia ndani ya chumba kile kilichowekwa mwili wa mtoto. Naye aliufungua mlango. Pale ndani alimwomba Mungu. Kwa uweza wa Mungu alirudishiwa uhai wake. Elisha alimwita mama wa yule mtoto. Naye alisema, "Mchukue mwanao" (2 Wafalme 4:36). Alikuwa hai tena.

Tunasoma maneno haya kutoka katika 2 Wafalme 4:37, "Ndipo akaingia, akamwangukia miguuni akainama mpaka nchi; kisha akamchukua mwanawe, akatoka." Tunaamini ya kuwa alimshukuru Mungu moyoni mwake.

**Sehemu ya Nne:** Kutii Maneno ya Nabii

Njaa ikaenea katika nchi ya Shunemu. Naye Elisha aliongea na yule mwanamke. Akamwambia aondoke aende pamoja na mwanaye katika nchi nyingine. Elisha alimwambia ya kuwa njaa itakaa kwa muda wa miaka saba. Naye alimtii yule nabii.

Baada ya muda wa miaka hiyo saba, alirudi katika nchi ya Shunemu. Naye alienda mbele za mfalme kumwomba arudishiwe shamba lake. Mfalme alikuwa akiongea na Gehazi akimwambia juu ya mambo makuu ambayo Elisha aliyafanya. Naye Gehazi akaanza kumwambia mfalme habari za mwanamke Mshunami. Alipokuwa akimwambia mfalme vile Elisha alivyomfufua mwanawe kutoka kwa wafu, wakati huo huo yule alifika kuuliza arudishiwe shamba lake. Naye Gehazi alisema, "Bwana wangu mfalme, huyu ndiye mwanamke, na huyu ndiye mwanaye, ambaye Elisha alimfufua" (2 Wafalme 8:5b). Naye mfalme akatoa amri kwamba arudishiwe nyumba na shamba lake. Naye alisema, "Mrudishie yote aliyokuwa nayo, na mapato yote ya shamba lake tangu siku aliposafiri, hata leo" (2 Wafalme 8:6b). Kwa kweli mwanamke huyo alikuwa na furaha moyoni mwake. Mungu alimtunza yeye pamoja na mtoto





Baadaye yule malaika akawaambia wale wanawake kwenda kuwaambia wanafunzi wake habari za kufufuka. Salome alikuwa na habari njema namna gani ya kuwaambia watu wengine. Siku hizi sisi pia tunayo habari njema ya kuwaambia watu wengine.

**Kiongozi:**

Daima Salome ataendelea kukumbukwa kama mama yao Yakobo na Yohana. Watu hawa wawili walikuwa watumishi wa kweli wa Mungu walio wakuu. Pia Salome alimtumikia Mungu, akiwa kwake nyumbani. Alikuwa akimtumikia Mungu alipokuwa akiwafundisha Yakobo na Yohana mambo ya Mungu.

Baadaye katika maisha yake, alikuwa mmoja wa wafuasi wa Yesu walio waaminifu. Alimtumikia kwa njia nyingi wakati Yesu alipokuwa akifundisha na kuhubiri. Yesu alipoangikwa wengi wa wanafunzi wake wakamtoroka. Lakini siyo Salome. Alisimama karibu na msalaba alipokufa. Yeye hakumwonea haya wala kuogopa. Salome alikuwa mmoja kati ya wale watu wa kwanza waliojua kuhusu kufufuka kwake Yesu.

Alikuwa amejifunza vyema kuhusu mambo yale yaliyokuwa yakifundishwa na Yesu. Ebu na sisi leo, tujifunze jambo hilo hilo. Na tumwombe Mungu ili amsaidie kila mmoja wetu kuwa mfuasi wake wa kweli.

**Sehemu ya Tatu:** Wakati wa Yesu Kusulibiwa

Tena Salome anaitwa "Mama yao wana wa Zebedayo." Yeye pamoja na wanawake wengine walimfuata Yesu kutoka Galilaya mpaka Yerusalemu na "kumtumikia." Soma Mathayo 27:55. Huko Yerusalemu Yesu aliteswa kwa mambo mengi. Alisulibiwa msalabani. Yeye hakutenda kosa lo lote. Alikufa kwa ajili ya dhambi za watu wote. Ukweli kuwa Salome alikuwa mmoja kati ya wale waliokuweko msalabani ni kwamba alikuwa mwaminifu katika kumfuata Yesu. Watu wengine wengi waliomsikia akihubiri walimtoroka. Lakini siyo Salome. Yeye aliendelea kuwa mfuasi hata wakati wa kufa.

**Sehemu ya Nne:** Wakati wa Kufufuka Kwake Yesu

Baada ya kufa kwake msalabani, mwili wa Yesu uliwekwa kaburini. Jiwe kubwa lilikuwa limevingirishwa mlangoni pa kaburi. Nao askari wakalilinda lile kaburi. Walifanya hivyo kwa sababu Yesu alikuwa amesema ya kuwa baada ya siku tatu atafufuka kutoka kwa wafu. Watawala walitaka kuhakikisha ya kuwa wanafunzi wake hawakuuiba mwili wa Yesu na kuwaambia watu, amefufuka kutoka kwa wafu.

Katika siku ya tatu alfajiri mapema, Salome na wanawake wengine wawili waliyanunua manukato. Walitazamia kwenda kuupaka mwili wa Yesu hayo manukato. Walipokuwa wakienda njiani walianza kuongea. Mmoja wao akauliza, "Ni nani atakayetuvingirishia lile jiwe mlangoni pa kaburi?" (Marko 16:3).

Tazama, walipofika jiwe lilikuwa limeshavingirishwa. Walipoingia ndani, walimwona mtu. Naye alikuwa malaika wa Bwana. Naye aliwaambia wanawake, "Mnamtafuta Yesu Mnazareti, aliyesulibiwa; amefufuka, hayupo hapa; patazameni mahali walipomweka" (Marko 16:6).





kwa muda wa miaka saba yenye njaa. Aliporudi nyumbani kwao, alirudishiwa vitu vyake vyote.

**Kiongozi:**

Leo tumejifunza habari za mwanamke ambaye alikuwa akiitwa "Mwenye cheo." Ukuu wake ulionekana katika njia ambayo kwayo aliweza kuyavumilia majaribu. Alikuwa na imani kuu katika majaribu mengi. Alikuwa akimtumikia Mungu katika imani yake.

Pia ukuu wake ulionekana katika njia ile aliyomsaidia Elisha. Ukuu wake ulionekana katika njia ile ambayo aliweza kukabili kifo.

Je! siku hizi sisi tu "wakuu" kwa njia ipi? Je! tunayo imani kubwa kwake Mungu? Je! tunaipenda kazi ya Mungu? Tunaposikia habari za kifo cha rafiki yule tumpendaye tunatenda vipi?

Ebu na tumwombe Mungu ili atusaidie katika mambo haya. Tukiwa peke yetu ni vigumu sana kuzishinda shida za maisha. Kwake Mungu yote yawezekana. Ni vigumu kumtumikia Mungu tukiwa peke yetu. Tutaweza kumtumikia Mungu kwa njia nyingi tukiwa pamoja naye.

FEBRUARI

Mpango wa Kwanza

## ELISABETI

**Kuyasoma Maandiko:** Luka 1:5-7

**Kifungu cha Kukumbuka:**

*"Nawe utakuwa na furaha na shangwe, na watu wengi watakufurahia kuzaliwa kwake."*

*Luka 1:14*

**Kiongozi:**

Leo tutaanza kujifunza kuhusu wanawake wa Agano Jipya walio wahudumu wa Mungu. Mojawapo wa wanawake hao wa kwanza ni Elisabeti. Elisabeti ndiye aliyekuwa mama wa Yohana Mbatizaji. Pia alikuwa mtu wa kwanza kumsalimu Mariamu mamaye Yesu.

**Sehemu ya Kwanza:** Maisha Yake

Elizabeti alikuwa mwanamke aliyempenda Mungu. Alikuwa ameshaolewa na Zakaria. Naye Zakaria alikuwa kuhani na alikuwa akihudumu Hekaluni. Katika Luka 1:6 twasoma habari za Elizabeti na Zakaria: "Na wote wawili walikuwa wenye haki mbele za Mungu, wakiendelea katika amri zote za Bwana na maagizo yake bila lawama."

Elisabeti na Zakaria wote wawili walikuwa wazee sana. Pengine walikaa miaka mingi tangu kuoana. Hawakuwa na watoto. Katika siku zile kila mwanamke wa Kiyahudi alikuwa akitamani kuwapata watoto katika nyumba yao. Wanawake hawakuheshimiwa na wanawake wengine wa kijiji mpaka walipozaa mtoto. Walakini, kutokuwa na mtoto hakukuwafanya Elisabeti na Zakaria kuwa na shaka kuhusu Mungu. Waliendelea kumwamini Mungu. Waliendelea katika kumwabudu na kumhudumu.





aliwaita ili wamfuate. Mathayo amesema ya kuwa, "Mara wakakiacha chombo na baba yao, wakamfuata" (Mathayo 4:22).

Tangu zamani, Salome hajulikani kama mke wa Zebedayo, bali anajulikana kama mama wa Yakobo na Yohana.

**Sehemu ya Pili:** Ombi Lake

Wakati wa kwanza wa kazi ya Yesu ya kuhubiri aliwachagua watu kumi na wawili. Watu hao walikuwa wakiitwa "Wanafunzi." Yakobo na Yohana walikuwa watu wawili kati ya hao kumi na wawili waliochaguliwa na Yesu. Salome akiwa kama wazazi wengine, alitamani wanawe wapate kilicho chema zaidi.

Watu wengi walikuwa wakifikiria kuwa Yesu alikuja kuuanzisha ufalme wake hapa ulimwenguni. Siku moja Salome alimwendea Yesu akiwa na ombi. Naye alimwuliza, "Wataka nini?" Naye alimjibu Yesu, "Agiza kwamba hawa wanangu wawili waketi mmoja mkono wako wa kuume, na mmoja mkono wako wa kushoto, katika ufalme wako" (Mathayo 20:21).

Naye Yesu alieleza jibu lake kwa hao wana wenyewe. Alisema, "Hamjui mnaloliomba. Je! mwaweza kunywea kikombe nitakachonywea mimi?" Nao wakamwambia, "Twaweza." Halafu Yesu akajibu swali la mama yao. Aliwaambia, "lakini kuketi mkono wangu wa kuume na mkono wangu wa kushoto, sina amri kuwapa, bali watapewa waliowekwa tayari na Baba yangu" (Mathayo 20:23).

Pengine Salome aliyahitaji maneno haya ya kumkemea ili ndipo aweze kujifunza hasa vile ukuu wa mambo ya kiroho huweza kupatikana katika kujinyima na katika kuwatumikia wengine. Yesu ametuambia ya kuwa "Bali mtu ye yote anayetaka kuwa mkubwa kwenu, na awe mtumishi wenu; na mtu ye yote anayetaka kuwa wa kwanza kwenu na awe mtumwa wenu" (Mathayo 20:26, 27).

### Mpango wa Tatu

## SALOME

**Kuyasoma Maandiko:** Marko 16:1-4

**Kifungu cha Kukumbuka:**

*"Akawaambia, enendeni ulimwenguni mwote, mkaihubiri Injili kwa kila kiumbe."*

*Marko 16:15*

**Kiongozi:**

Leo tutajifunza habari za mwanamke aliyeitwa Salome. Salome ndiye aliyekuwa mama yake Yakobo na Yohana. Wakati wavulana hao wawili walipokuwa wazima, walikuwa wawili kati ya wanafunzi wa Yesu. Tunaona ya kuwa Salome alimtumikia Yesu kwa njia kadha. Pengine utumishi wake ulio mkuu ulikuwa nyumbani mwake.

**Sehemu ya Kwanza:** Akiwa Mzazi

Katika Mathayo 20:20 na Mathayo 27:56 yule mtu tunayejifunza habari zake anaitwa, "Mama yao wana wa Zebedayo." Katika sehemu hizi mbili haitwi Salome. Katika Marko 15:40 na Marko 16:1 ameitwa kwa jina lake, Salome.

Salome alikuwa mke wa Zebedayo. Nyumbani kwao kulikuwa pwani ya bahari ya Galilaya. Zebedayo alikuwa mvuvi. Aliwaajiri watu waliomsaidia yeye pamoja na wanawe. (Tazama Marko 1:19-20). Hii ni kuonyesha kuwa Zebedayo alikuwa mtu mwenye mali nyingi.

Inaonekana kuwa Salome aliwafundisha wanawe mambo ya Mungu. Huenda aliwaambia habari za Mwokozi aliyeahidiwa. Wakati Yesu alipokuwa akiwachagua wanafunzi wake alipitia karibu na nyumbani kwa Yakobo na Yohana. Naye





**Sehemu ya Pili:** Neno la Mungu kwa Zakaria

Siku moja Zakaria alikuwa akifanya kazi ya Mungu hekaluni. Naye malaika wa Mungu alimtokea. Zakaria alipomwona yule malaika alifadhaika moyoni.

Naye malaika akamwambia, "Usiogope, Zakaria, maana dua yako imesikika, na mkeo Elisabeti atakuzalia mtoto, na jina lake utamwita Yohana" (Luka 1:13) Naye Zakaria alishangaa sana. Lilikuwa jambo gumu kuliamini. Naye Zakaria alimwuliza yule malaika, "Nitajuaje neno hilo? Maana mimi ni mzee, na mke wangu ni mkongwe wa siku nyingi" (Luka 1:18).

Naye malaika alimhakikishia Zakaria kuwa alikuwa akinena neno la Mungu. Naye alikuwa ametumwa na Mungu kumletea Zakaria ujumbe. Ukiwa kama ushahidi, malaika alisema, "Na tazama! utakuwa bubu, usiweze kusema, mpaka siku ile yatakapotukia hayo, kwa sababu hukuyasadiki maneno yangu; nayo yatatimizwa kwa wakati wake" (Luka 1:20).

Hatuelewi vile Elisabeti alivyofanya wakati mumewe alipomwambia habari. Walakini, tutaweza kufikiria kuwa alifurahi sana. Mwishowe alimpata mtoto. Tutaweza kufikiria kuwa alimshukuru Mungu kwa kuyajibu maombi yake.

**Sehemu ya Tatu:** Elisabeti na Mariamu

Wakati Elisabeti alipotimiza miezi sita akimngojea mtoto azaliwe, malaika Gabrieli alitumwa kwenda kwa mtu mwingine. Wakati huu alimwendea Mariamu. Akamwambia kuwa angekuwa mama yake Yesu. Tena akamwambia kuwa binamu yake Elisabeti alikuwa akitarajia kumzaa mtoto. Soma Luka 1:36. Naye Mariamu aliondoka akaenda mpaka nyumbani kwa Elisabeti. Baada ya kufika kule, Mariamu alimwamkia Elisabeti. Mara Elisabeti alitambua ya kuwa Mariamu angekuwa mama wa Yesu. (Soma Luka 1:36).

Mariamu alikaa na Elisabeti kadiri ya miezi mitatu. Katika Biblia hatuambiwi juu ya mambo yale waliyofanya wakati wa muda huo. Tutaweza kufikiria tu kuwa waliongea kuhusu mambo mengi. Pengine walikuwa na furaha walipokuwa wakipanga kuhusu kuzaliwa kwa watoto wao.

Mwisho wa muda wa miezi mitatu, Mariamu alirudi kwao nyumbani. Halafu, Elisabeti alimzaa mwana.

**Sehemu ya Nne:** Elisabeti na Mwanawe

Siku zile mtoto alikuwa akipewa jina baada ya siku nane tangu kuzaliwa. Marafiki na jamaa walikuja kumsalimu Elisabeti katika siku ya nane baada ya kuzaliwa kwa mwanawe. (Soma Luka 1:59). Watu wengine walisema ya kuwa jina la mtoto lingekuwa ni "Zakaria," kufuatana na jina la babaye. Naye Elisabeti alijibu, "La, ni lazima aitwe Yohana." Jamaa zake hawakuweza kufahamu maana ya jina hili. Kisha walimwuliza Zakaria kuhusu jina la mtoto. Tangu wakati ule malaika aliposema na Zakaria, Zakaria alikuwa hawezi kutamka neno.

Zakaria alionyesha ishara kwamba alipenda kuandika jambo. Halafu aliandika kwa kusema, "Jina lake ni Yohana" (Luka 1:63). Na papo hapo kinywa chake kilifunguka na aliweza kusema tena. Na alimsifu Mungu.

Biblia haituelezi kuhusu maisha ya Yohana akiwa mvulana. Tunasoma tu, "Yule mtoto akakua, akaongezeka nguvu rohoni..." (Luka 1:80). Tunaweza kufikiria ya kuwa Elisabeti alimfundisha mambo ya Mungu. Alimfundisha juu ya kumwamini Mungu sana.

Yohana Mbatizaji ndiye aliyemtangulia Yesu. Naye aliwaambia watu habari za kuja kwa Yesu. Naye aliitengeneza njia kwa ajili ya Yesu. Kazi ya Yohana Mbatizaji ilikuwa kazi ya Yesu.





**Kiongozi:**

Leo tulipokuwa tukijifunza habari za Ana, tumejifunza mambo fulani. Kwanza, tumeona ya kuwa Ana hakupungukiwa na tumaini kuhusu kuja kwa Yesu. Watu wengi walikuwa wameshapoteza tumaini hilo. Lakini siyo Ana. Alikuwa ameyajua maneno ya Mungu kutoka katika Agano la Kale. Alikuwa amemwamini Mungu sana.

Wakati alipojua ya kuwa ahadi ya Mungu imeshatimizwa, aliwaambia watu wengine. Tukipata kuzijua habari njema siku hizi, sisi huwaambia rafiki zetu. Je! hivyo si kweli? Ni habari njema zaidi namna gani tunazoweza kuwaambia zaidi habari za Yesu Kristo. Ni lazima tuwaambie wengine habari za wokovu upatikanao katika Kristo.

Ebu na tumwombe Mungu ili atusaidie sisi pia tunapowaambia wengine habari zake.

**TANGAZO:**

Juma la kwanza la Machi ni Juma la Maombi. Anza sasa kupanga kukutana na kuomba.

**Sehemu ya Tatu:** Tumaini Lake Kutimizwa

Yesu alizaliwa nayo ahadi ikatimizwa. Yesu alipokuwa na umri wa siku arobaini, Mariamu na Yusufu walienda hekaluni katika Yerusalemu. Na walienda pamoja na mtoto Yesu. Hii ilikuwa kwa namna ya desturi za Waisraeli. Hekaluni kulikuwa na mzee mmoja jina lake Simeoni. Naye pia, alikuwa akitazamia kuja kwa Masihi. Roho Mtakatifu alikuwa amemfunulia Simeoni kwamba hatakufa kabla ya kumwona Yesu.

Wakati Mariamu na Yusufu walimpeleka Yesu Hekaluni, Simeoni alimpokea Yesu mikononi akisema, "Sasa, Bwana, wamruhusu mtumishi wako, kwa amani, kama ulivyosema; kwa kuwa macho yangu yameuona wokovu wako" (Luka 2:29-30).

Wakati uo huo Simeoni alipokuwa akiongea, naye Ana aliingia hekaluni. Na yeye pia, alijua ya kuwa ahadi ya Mungu imetimizwa. Alimshukuru Mungu kwa sababu ya kuzaliwa kwa Mwokozi, Yesu Kristo. Yeye alikuwa ameishi ili ndipo amwone Mwokozi.

**Sehemu ya Nne:** Kuwaambia Wengine "Habari Njema."

Katika Yerusalemu kulikuwa na watu wale waliokuwa wakingojea kuja kwa Yesu. Ana, nabii mke, alipata kumwona Yesu kwa macho yake mwenyewe. Alijua ya kuwa alikuwa amekwisha zaliwa. Alifahamu ya kuwa ahadi imekamilishwa. Kwa hivyo, aliweza kuwaambia watu wote juu ya kuzaliwa kwa Yesu. Pengine alikuwa akisema kwa mtu mmoja mmoja. Au pengine alisema nao walipokuwa wakija hekaluni. Vile tujuavyo ni kwamba alisema na watu wale aliowajua kuwa walikuwa wakingojea kuja kwa Yesu.

Je! siku hizi tunawaambia marafiki zetu habari za Yesu?





**Kiongozi:**

Pengine Elisabeti alimtumikia Mungu kwa njia nyingi. Ebu na tukumbuke juu ya njia mbili ambazo kwa hizo aliweza kumtumikia Mungu. Alimtumikia Mungu akiwa kwake nyumbani. Alikuwa na imani kubwa kwake Mungu.

Halafu Elisabeti alimtumikia Mungu akiwa mama yake Yohana Mbatizaji. Hakika alimfundisha mambo ya Mungu. Alisaidia katika kumfunza Yohana mambo ya Mungu.

Je! siku hizi tutaweza kumtumikia Mungu kwa njia zipi ambazo ni bora zaidi? Tukiwa kama Wakristo, ni lazima nyumba zetu ziwe mfano mwema kwa ajili yake Mungu. Pia tunapaswa kutafuta njia za kuwafundisha watoto wetu mambo ya Mungu. Tuwasaidie katika kuwatayarisha kumtumikia Mungu katika jamaa zao, makanisa yao, na kuwatumikia watu wa jamii wanaoishi pamoja nao.

Na tumwombe Mungu atusaidie ili ndipo tumtumikie katika njia hizi.

Mpango wa Pili

## ANA

**Kuyasoma Maandiko:** Luka 2:36-38

**Kifungu cha Kukumbuka:**

*"----Mwimarike, msitikisike, mkazidi sana kutenda kazi ya Bwana siku zote, kwa kuwa mwajua ya kwamba taabu yenu siyo bure katika Bwana."*

*1 Wakorintho 15:58*

**Kiongozi:**

Kuna mistari mitatu tu katika kitabu cha Luka, sura ya pili, ambayo yatueleza habari za Ana. Hata ingawa hivyo, tutajifunza mambo fulani kutoka katika maisha ya mwanamke huyu ambaye alimhudumia Mungu kwa muda wa miaka mingi iliyopita. Yeye alikuwa mwanamke mwenye imani kubwa. Ebu na tujifunze kutoka katika maisha ya Ana.

**Sehemu ya Kwanza:** Siku za Maisha Yake

Kwa muda wa miaka mia kadha, watu walikuwa wakingojea juu ya kuja kwa Masihi. Ahadi ya kuja kwa Mwokozi ilipewa kwao Adamu na Hawa. Walipotenda dhambi wakiwa katika Bustani ya Edeni, Mungu alitoa ahadi ya kumleta Mwokozi. (Soma Mwanzo 3:15). Katika Agano la Kale lote tunaona ahadi hii ikirudiwa kwa ajili ya wana wa Israeli. Nayo miaka mingi ilipita. Nao watu walichoka hawakuwa na tumaini la kuzaliwa kwake Masihi aliyeahidiwa. Ana alikuwa akiishi nyakati hizi.

Ana alikuwa nabii mke. Tunakumbuka ya kuwa nabii mke alikuwa ndiye aliyehusika na kuwaambia watu Neno la Mungu. Luka ametuambia kutoka katika sura ya 2 na kifungu cha 37





habari za Ana. "Haondoki, katika hekalu, ila huabudu usiku na mchana kwa kufunga na kuomba." Yeye alimpenda Mungu zaidi ya mambo mengine yote.

Pia Ana alikuwa mwanamke mkongwe. Naye alikuwa ameolewa na kukaa na mumewe kwa muda wa miaka saba tu. Kisha mumewe akafa. Hakuolewa tena. Biblia haituambii habari za watoto wao. Kwa hivyo tutaweza kudhania ya kuwa labda hakuwa na watoto.

**Sehemu ya Pili:** Tumaini Lake

Watu wengi wa nyakati za Ana walikuwa wameshakoma kutazamia kuja kwa Mwokozi aliyeahidiwa. Kulikuwa na dhambi nyingi kila mahali nchini. Ingawa hivyo, Ana pamoja na kundi lingine la watu waliendelea kutazamia kuja kwa Mwokozi. Kama ilivyokuwa kwa watu wote wa kale, hawakujua ni lini ile ahadi itatimizwa. Jambo la maana lilikuwa kwamba hawakupoteza tumaini lao.

Tukiwa kama Wakristo, siku hizi tunatazamia kurudi kwake Kristo kwa mara ya pili. Kunao watu wengi wanaotuzunguka ambao wao si Wakristo. Baadhi ya watu hao hudhihaki imani na tumaini la Wakristo.

Pia tunaona dhambi kila mahali. Watu hawa hawajali juu ya kurudi kwa pili kwake Kristo. Hawajali juu ya uzima baada ya kufa kwa miili yao. Wanafikiria tu juu ya anasa za ulimwengu huu. Mambo haya yasiwafanye Wakristo kupoteza tumaini lao. Ni lazima tudumu katika mambo ya Mungu. Ahadi ya kurudi kwa Kristo ni lazima itatimizwa. Kama ilivyokuwa kwa Ana hapo kale, sisi tulio wa siku hizi hatujui ni lini ahadi itakapotimizwa. Ni lazima kujitayarisha.